**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2019/2020; PAMOJA NA MAONI NA USHAURI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2020/2021

---

*[Imeandikwa kwa mujibu wa Kanuni ya 123 na kuwasilishwa Bungeni kwa Mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

IDARA YA KAMATI ZA BUNGE,
S.L.P. 941,
**DODOMA**.

**MEI, 2020**

## YALIYOMO

**YALIYOMO** ........................................................................................................ i
**SEHEMU YA KWANZA** ........................................................................................ 1
1.0 **UTANGULIZI** .................................................................................................. 1
**SEHEMU YA PILI** .................................................................................................. 3
2.0 **MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021** ........................................................ 3
2.1 Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka 2019/2020 ............................................ 3
2.2 Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2019/2020 ............................................ 3
2.3 Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2019/2020 ........................................................................................ 5
2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati ............................................ 11
2.5 Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ........................................................................................ 15
2.5.1 Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ........................................................................ 15
2.5.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ........................................................................ 15
2.6 Mambo Mengine yaliyojitokeza wakati wa Kupita na Kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2020/2021 ............ 16
**SEHEMU YA TATU** ............................................................................................ 32
3.0 **MAONI NA USHAURI WA KAMATI** ........................................................ 32
3.1 Bajeti ya Wizara ........................................................................................ 32
3.2 Sekta ya Uchukuzi ..................................................................................... 32
3.3 Sekta ya Ujenzi ......................................................................................... 37
3.4 Sekta ya Mawasiliano ................................................................................. 40
4.0 **HITIMISHO** ............................................................................................... 44
4.1 Shukrani .................................................................................................... 44
*KIAMBATISHO NA.1,* Gharama zilizolipwa na zinazodaiwa na Wakala wa Majengo za Ada ya Ushauri kwa Wizara na Taasisi zilizojenga Ofisi Mtumba, Dodoma ................................................................................................ 47

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020; PAMOJA NA MAONI NA USHAURI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia Kanuni ya 123 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, sehemu hii inabainisha mpangilio wa taarifa inayowasilishwa;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi unaojikita katika masuala makubwa mawili yafuatayo: -

    i) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2019/2020. Mapitio yanajielekeza zaidi katika makusanyo ya mapato, upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo, ukaguzi wa miradi ya maendeleo na utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati;

    ii) Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Uchambuzi huu upo katika maeneo makuu matatu ambayo ni Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Mambo mengine

yaliyojitokeza wakati wa kupitia na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2020/2021.

c) Sehemu ya Tatu imejielekeza katika Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusiana na masuala yote yaliyofanyiwa uchambuzi katika **Fungu 62 (Sekta ya Uchukuzi), Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi)** na **Fungu 68 (Sekta ya Mawasiliano).**

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

### 2.1 Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Sekta ya Mawasiliano (Fungu 68), liliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 22,517,437,400** kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Hadi kufikia 29 Februari, 2020, zimekusanywa **Shilingi 15,273,525,046** sawa na **asilimia 68** ya makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, fungu 98- Sekta ya Ujenzi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 68,828,000.00** kupitia idara zenye vyanzo vya mapato. Idara hizo ni Idara ya Utawala, Idara ya Huduma za Ufundi na Kitengo cha Menejimenti ya Manunuzi. Hadi kufika mwezi Februari, 2020 jumla ya **Shilingi 23,790,000.00** zilikuwa zimekusanywa sawa na **asilimia 34.56** ya malengo ya makusanyo ya sekta hii kwa mwaka wa fedha 2019/20.

### 2.2 Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** kipengele hiki kinabainisha upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa Sekta zote za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Jedwali Na. 1, Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hadi Kufikia Februari, 2020**

| SEKTA | Fedha zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2019/20 | | | Fedha zilizotolewa hadi kufikia Februari, 2020 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Matumizi ya Kawaida | Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo | Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo | Matumizi ya Kawaida | Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo | Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo |
| Uchukuzi | 85,408,131,000 | 3,327,716,600,000 | 216,005,642,895 | 53,404,102,071.14 (62%) | 863,848,881,683 (26%) | 145,201,000,000 (67%) |
| Ujenzi | 36,245,250,004.04 | 1,081,219,351,229.52 | 304,051,604,268.00 | 22,091,947,758.04 (60.95) | 586,419,296,780.16 (54%) | 275,991,529,676.01 (91) |
| Mawasiliano | 3,973,197,000 | 0 | 0 | 2,481,463,936 (62.4) | 0 | 0 |

***Chanzo: Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano 2019/2020***

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62), katika mwaka wa fedha 2019/2020 iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi Trilioni 3.6 (3,629,130,373,895).** Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 85.4 (85,408,131,000)** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Trilioni 3.5 (3,543,722,242,895)** fedha za Miradi ya Maendeleo. Fedha zilizotolewa hadi kufikia mwezi Februari, 2020 ni **Shilingi Trilioni 1.0 (1,009,049,881,683)** sawa na **asilimia 28** ya fedha zote zilizoidhinishwa. Kamati imeendelea kubaini kuwapo kwa changamoto ya kutokutolewa fedha kwa wakati kwa Sekta hii na kusababisha baadhi ya miradi kuchelewa kuanza na kukamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Ujenzi (Fungu 98), katika mwaka wa fedha 2019/2020 iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi Trilioni 1.4 (1,421,516,205,501.56**). Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 36.1** (**36,142,664,000.00**) ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Trilioni 1.3 (1,385,270,955,497.52)** fedha za Miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, fedha za matumizi ya kawaida imeongezewa wigo kutoka **Shilingi bilioni 36.1 (36,142,664,000.00)** zilizoidhinishwa na Bunge mpaka **Shilingi bilioni 36.2 (36,245,250,004.04).** Hili ni ongezeko la **Shilingi milioni 102,586,004.04.** Ongezeko hili ni kwa ajili ya malipo ya madeni ya Wazabuni mbalimbali ambayo yamehakikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Hadi kufikia mwezi Februari, 2020 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi bilioni 862.4 (862,410,826,456.20)** sawa na **asilimia 62.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, pamoja na fedha kutolewa kwa Sekta ya Ujenzi kwa **asilimia 62**, hadi mwezi Machi, 2020 ilipokuwa ikichambua bajeti ya Sekta ya Ujenzi, baadhi ya miradi hasa ya ujenzi wa viwanja vya ndege haikuwa imepata fedha yoyote. Viwanja vya ndege hivyo ni Kiwanja cha Ndege cha Kigoma, Mpanda, Tabora, Shinyanga, Sumbawanga, Songwe, Kilimanjaro na Arusha. Aidha, baadhi ya miradi ya barabara nayo haikupata fedha, miradi hiyo ni pamoja na barabara ya Singida-Babati-Minjingu, Same-Mkumbara-Korogwe, Arusha-Namanga, Mafia *Airport Access Road*, Korogwe-Handeni, Mwanza-Shinyanga Border, Dar es Salaam-Chalinze-Morogoro *Express Way*.

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Mawasiliano (Fungu 68), mwaka wa fedha 2019/2020 iliidhinishwa jumla ya **Shilingi Bilioni 3.9 (3,973,197,000)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi mwezi Februari, 2020 Sekta ya Mawasiliano imepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 2.4 (2,481,463,936)** sawa na **asilimia 62.4**. Katika fungu hili hakukutengwa fedha za miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa fedha hizo za miradi ya maendeleo zingetolewa toka katika fedha za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.Kamati imebaini kuwa fedha hizo za miradi ya maendeleo hazikutolewa kama zilivyokuwa zimehaidiwa na hivyo kusababisha miradi kutokutekelezwa.

## 2.3 Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyokuwa imetengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Ziara hii ilifanyika kuanzia tarehe 12 hadi 19 Machi, 2020 katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam. Miradi iliyotembelewa ni; -

i. Mradi wa ujenzi wa Ofisi za Serikali Ihumwa-Dodoma;
ii. Mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa (*standard guage)* sehemu ya Dar es Salaam -Morogoro na Morogoro –Dodoma;
iii. Mradi wa ujenzi wa barabara ya juu *(Ubungo Interchange);*
iv. Mradi wa ujenzi wa nyumba za Magomeni;
v. Mradi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka (BRT)
vi. Mradi wa ujenzi wa bandari ya Dar es Salaam; na
vii. Mradi wa Ujenzi wa daraja la mto Wami.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya miradi iliyokuwa katika ratiba ya Kamati haikutembelewa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Corona (virusi vya *Covid 19*). Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa daraja la *Selander*, Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na Jengo la tatu la abiria *(terminal III)* katika Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere.

**i) Ujenzi wa Ofisi za Serikali- Mtumba, Dodoma**

**Mheshimiwa Spika**, mwezi Septemba, 2016, Serikali ilifanya maamuzi ya kuhamishia shughuli za Serikali jijini Dodoma kama sehemu ya kukamilisha ndoto ya siku nyingi iliyowekwa na Baba wa Taifa Hayati Mwalim Julius Kambarage Nyerere mwaka 1973. Serikali ilitenga sehemu maalum eneo la Mtumba jijini Dodoma ambako ilielekeza yajengwe majengo ya ofisi yatakayotumiwa na Wizara mbalimbali pamoja na baadhi ya taasisi zake. Mnamo mwezi Juni, 2018, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ulielekezwa na Serikali kufanya ubunifu na usanifu wa mji huu kwa kuzingatia mahitaji ya wizara husika. Wajibu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) katika mradi huu ulikuwa ni Mshauri elekezi katika hatua za awali na usimamizi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa majengo yote 21 ya awali isipokuwa la TAMISEMI yalijengwa kwa gharama ya chini ya **Shilingi Bilioni 1** (VAT ikiwemo) bila kuhusisha kazi za nje na kazi za TEHAMA. Aidha, kutokana na ufinyu wa bajeti kazi za mtandao wa viyoyozi hazikufanyika kwa majengo yote.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa katika mradi wa ujenzi wa Ofisi za Serikali ni Washitiri kutokumlipa Wakala wa Majengo Tanzania-TBA ada ya ushauri licha ya kuwa huduma husika zimetolewa. Mpaka Kamati ilipotembelea mradi huu mwezi Machi, 2020, Kiasi cha ada ya ushauri kilicholipwa ni **Shilingi Milioni 447.9 (447,904,180.85)** na deni lililosalia ni **Shilingi Bilioni 1.26** (**1,260,437,182.44)**. Kwa mwenendo huu, Kamati inaona kwamba nguvu na kasi ya Wakala wa Majengo Tanzania vinazoroteshwa, na hivyo, kuathiri moja kwa moja utendaji kazi wa Wakala hasa ukizingatia Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara kuwa Wakala huu uweke mkakati wa kujiendesha kibiashara na kuachana na utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** *kiambatisho Na. 1* kinaonesha mchanganuo wa Gharama za Ada ya Ushauri zilizolipwa na zinazodaiwa na Wakala wa Majengo Tanzania kwa Wizara zilizojenga Ofisi eneo la Mtumba, Dodoma

### ii) Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kisasa (*standard guage)* sehemu ya Dar es Salaam- Morogoro na Morogoro –Dodoma

**Mheshimiwa Spika**, maendeleo ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa *(standard guage)* ni mazuri kwani hadi mwezi Machi, 2020 Kamati ilipotembelea mradi huu kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300), ujenzi umefika asilimia sabini na tano (75%). Shughuli zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa makalvati, ambao umefikia asilimia 97, ujenzi wa daraja refu katikati ya jiji la Dar es Salaam lenye jumla ya km 2.54 umefikia asilimia 85, wakati ukataji wa miinuko na ujazaji wa mabonde umefikia asilimia 83.

Vilevile, mkataba umesainiwa kwa ajili ya ujenzi wa mfumo wa umeme wa SGR ambapo kazi imefikia asilimia 7. Kamati imejulishwa kuwa kwa kipande cha Dar es Salaam- Morogoro kazi zote zinatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu sehemu ya pili kutoka Morogoro hadi Makutopora -Dodoma (km 422), ambapo ujenzi umefikia asilimia 28 (28%). Kazi zinazoendelea ni pamoja na ukataji wa miinuko na ujazaji wa mabonde, usanifu wa njia, ujenzi wa mahandaki, pamoja na uthamini na uhakiki wa mali za wananchi watakaopisha mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa jumla, maendeleo ya mradi kutoka Dar es Salaam -Morogoro –Dodoma ni mazuri, kwani fedha kwa ajili ya malipo mbalimbali ya mradi zinatolewa kwa wakati na hakuna madai yoyote kwa Mkandarasi. Aidha, fidia mbalimbali kwa ajili ya maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa reli zinaaendelea kutolewa kadiri mradi unavyosogea. Kamati inasisitiza umuhimu wa kuwa na wataalam wa kutosha wa ndani ili waweze kuwa na ujuzi wa kutosha kusimamia na kuendeleleza reli hii.

### iii) Mradi wa ujenzi wa barabara ya juu *(Ubungo Interchange)*

**Mheshimiwa Spika**, Ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya eneo la Ubungo jijini Dar es Salaam (*Ubungo Interchange)* una lengo la kupunguza msongamano wa magari, kwa kutenganisha njia za barabara za Morogoro,

Mandela na Sam Nujoma. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia kwa kiasi cha **Dola za Kimarekani Milioni 86** na Serikali imechangia fedha za fidia kwa waathirika wa Mradi. Kwa jumla maendeleo ya iutekelezaji wa mradi hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2020 yamefikia asilimia 70.

Kamati imefarijika kwa kujulishwa mradi huu umeajiri wazawa wengi ambapo jumla ya wafanyakazi wote ni 960 na wazawa ni asilimia 90. Daraja linatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2020.

### iv) Mradi wa ujenzi wa nyumba za Magomeni

**Mheshimiwa Spika,** nyumba za Magomeni zilijengwa na Wakoloni mwishoni mwa miaka ya 1940 na mwanzoni mwa miaka ya 1950 kufuatia mahitaji ya Waafrika waliokuwa wanafanya kazi maeneo ya Oysterbay, Dar es Salaam. Mnamo tarehe 06 septemba 2016, Mhe Rais Dk. John Pombe Magufuli aliwatembelea waliokuwa wapangaji wa Magomeni hizi na kutoa ahadi ya kuwajengea makazi mapya. Lengo lilikuwa kuzipatia makazi bora familia **644** za waliokuwa wakazi wa nyumba hizo kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 20 (20,000,000,000).** Mradi unajumuisha ujenzi wa nyumba za makazi zenye huduma zote za jamii, uzio, miundombinu na mandhari ya nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imejulishwa kuwa ujenzi wa mradi huu ulianza tarehe 01 Octoba,2016 ambapo ulitarajiwa kumalizika katika kipindi cha mwaka mmoja (wiki 52) yaani 31 Septemba 2017. Hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo za kifedha, mradi ulisimama kwa vipindi tofauti kuanzia mwaka 2017. Hivyo, kwa sasa, utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia Sabini (70%) ambapo zinahitajika **Shilingi Bilioni 14 (14,742,034,302.60)** ili mradi uweze kukamilika ifikapo mwezi June, 2020.

### v) Mradi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka (BRT)

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Usafiri wa Haraka wa Mabasi (BRT) Awamu ya Pili, ni muendelezo wa mkakakati wa kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam. Mkakati huu unalenga kujenga mradi katika awamu sita ambapo awamu ya Kwanza ilihusisha ujenzi

wa barabara za Morogoro kutoka Kimara hadi Kivukoni; Kawawa kutoka Magomeni hadi Morroco; na Mtaa wa Msimbazi kutoka Fire hadi Kariakoo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea ujenzi wa miundombinu ya Usafiri wa Haraka wa Mabasi (BRT) Awamu ya Pili ambao unahusisha barabara ya Kilwa (Kamata hadi Mbagala), barabara ya Changombe/Kawawa (Magomeni hadi Mgulani) na barabara ya Sokoine (Gerezani – *City hall*). Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo kiasi cha **Dola za Kimarekani Milioni 141.71** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na Mfuko wa pamoja wa Maendeleo ya Afrika pamoja na Serikali kuchangia kiasi cha **Dola za Kimarekani Milioni 17.61** kwa ajili ya fidia. Hivyo, jumla kiasi cha fedha za Mradi huu ni **Dola za Kimarekani Milioni 159.32**. Eneo lilikabidhiwa kwa mkandarasi tarehe 1 Machi 2019 na alianza kazi rasmi tarehe 6 Mei 2019. Kwa sasa, Mkandarasi amekamilisha kuandaa vifaa vya ujenzi na anaendelea na kazi za awali za barabara. Kwa ujumla, kazi imefikia asilimia 2.8 ukilinganisha na asilimia 15.6 iliyopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kukagua mradi wa barabara za mabasi yaendayo kasi awamu ya pili, Kamati iliitaka Serikali kuangalia upya changamoto inayoendelea kujitokeza katika awamu ya kwanza kwa kipande cha Magomeni hadi *Fire* ambapo mto Msimbazi umekuwa ukijaza maji barabarani kiasi cha magari ya mradi kushindwa kupita na yale yaliyopo katika kituo cha mabasi *(depot)* kuharibika kutokana na kuingia maji.

**vi) Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Dar es Salaam**

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu Kamati inaipongeza Serikali kwani ilipotembelea Bandari ya Dar es Salaam mnamo mwezi Machi, 2020 ilijionea maendeleo ya miradi ya ujenzi na upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam ikiwa inaendelea vizuri.

**Mheshimiwa Spika,** Uboreshaji wa gati namba 1-7 na ujenzi wa gati jipya la kushushia magari.

Kamati imejionea kazi zilizokamilika bandarini hususan ujenzi wa gati la kushushia magari *(RoRo Berth)*, ujenzi wa gati namba 1, 2, na 3 pamoja na eneo la kuegesha magari. Kazi zinazoendelea ni uimarishwaji na kuongeza kina cha gati

namba 4,5, na 6 ambapo mwishoni mwa mwezi Machi, 2020 Mkandarasi anatarajiwa kukamilisha gati namba 4 pamoja na eneo lote la kuegesha magari yanayoshushwa katika gati la *RoRo*. Kwa ujumla kazi ya maboresho ya gati namba 1-7 pamoja na gati jipya la RoRo umefikia asilimia 71.2.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu upanuzi na kuchimba ili kuongeza kina cha lango la kuingilia meli*.* Kamati imejulishwa kuwa Mkataba kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania na Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu juu ya namna bora ya kupanua na kuchimba ili kuongeza kina cha lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli ulisainiwa mwezi Desemba, 2015 na kukamilika mwezi Machi, 2017. Kazi ya usanifu wa awali ilianza mwezi Desemba, 2018 na kukamilika mwezi Juni 2019. Kwa sasa hatua za manunuzi kumpata Mkandarasi wa kazi hii zinaendelea na kazi zinatarajiwa kuanza mwezi Aprili,2020 na kukamilika ndani ya miezi 30.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu kuimarisha gati namba 8-11, Mamlaka ya Bandari ipo katika hatua za kufanya tathimini ya zabuni ambapo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2020.

Aidha, Kamati imejulishwa kuwa awamu ya pili ya mradi wa uboreshaji wa bandari itajumuisha ujenzi wa matenki ya kuhifadhia mafuta pamoja na gati la mafuta pamoja na gati la kupakulia mafuta. Vilevile itahusisha ujenzi wa gati la makasha kuanzia gati namba 12-15, ujenzi wa gati la meli za kitalii na ujenzi wa gati kwa ajili ya meli za mwambao na Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilijionea eneo la Kurasini *Oil Jet* ambalo lilikuwa linaandaliwa kwa ujenzi na ukarabati wa eneo linalotarajiwa kufungwa *flow meter* ambapo Kamati ilijulishwa kuwa *flow meter* ya bandari ya Dar es Salaam ni kati ya flow meter tatu zilizoingiwa mkataba wa manunuzi kwa ajili pia ya Bandari za Tanga na Mtwara ambazo zinatarajia hadi mwezi Julai, 2020 mitambo hiyo itakuwa imefungwa.

**vii) Mradi wa Ujenzi wa daraja la mto Wami**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati litembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa daraja jipya la Wami lenye urefu wa mita 510 upana wa mita 11.85 linalojengwa na Mkandarasi *Power Construction Corporation Ltd* kwa gharama ya **Shilingi Bilioni**

**68**. Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 28 Juni, 2018 na tarehe ya kumaliza kazi ni 21 Oktoba, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kujenga daraja jipya kwani daraja lililopo halikidhi mahitaji ya sasa kwa kuwa ni jembamba na lenye njia moja ambayo iko kwenye miinuko mikali na kona pamoja na changamoto ya wingi wa magari na hivyo kusababisha ajali mara kwa mara.

## 2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/20, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali. Maoni na ushauri huo uligusa masuala muhimu kama vile Bandari, Reli, Viwanja vya Ndege, Barabara na Mawasiliano. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya mambo yaliyoshauriwa, yapo ambayo Serikali imeyazingatia na mengine yanaendelea kuzingatiwa. Baadhi ya ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni pamoja na: -

### a) Sekta ya Uchukuzi

i) Kuhusu ushauri wa ujenzi wa Reli ya Kati kwa kuzingatia kipaumbele kwenye reli yenye matarajio ya mzigo mkubwa ili kutengeneza mazingira ya Serikali kurudisha fedha zilizotumika ndani ya muda mfupi. Kamati imefarijika kujulishwa kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya SGR umekamilika kwa vipande vya Isaka – Rusumo (Km 371) Tabora – Kigoma (Km 411), Keza - Ruvubu (Km36), na Kaliua – Mpanda - Karema (Km 321). Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli hizo kwa kiwango cha SGR.

ii) Kuhusu Shirika la Reli Tanzania (TRC) kujiendesha kisasa kwa kufunga vyombo vya kielektroniki ili kuweza kutunza kumbukumbu zote za kiutendaji, ufuatiliaji wa mizigo kwa wateja, udhibiti mafuta, udhibiti wa mwendo na usalama. Kamati imejulishwa kuwa Shirika la Reli Tanzania limeanza ufungaji wa mifumo ya kielektroniki ya ukatishaji tiketi *(e-ticketing)* umeanza kutumika ambapo hadi Februari, 2020 jumla ya stesheni 71 zimefungiwa mfumo huo kwa lengo la kuboresha ukusanyaji wa mapato.

iii) Kuhusu Serikali kushirikisha sekta binafsi au kupata mikopo yenye gharama nafuu ili kuharakisha ujenzi wa reli nchini. Kamati imejulishwa kuwa Serikali inatarajia kujenga reli ya Mchuchuma – Liganga (Km 1,092. Baada ya mshauri mwelekezi kushindwa kutekeleza kazi ya kuunadi mradi, taratibu za kuvunja mkataba zimeendelea na imeundwa Kamati ya wataalam kushughulikia chini ya utaratibu wa *PPP*. Kuhusu reli ya Tanga – Arusha – Musoma (Km 1,108) kwa mwaka 2019/2020 taratibu za kuajiri mtaalam wa uwekezaji atayeandaa andiko la kuunadi mradi kwa wawekezaji kwa mfumo wa ubia *(PPP)*.

iv) Kuhusu Serikali kurasimisha Bandari Bubu zilizopo katika mwambao wa Bandari ya Hindi na katika Maziwa Makuu ili kuongeza mapato. Kamati imejulishwa kuwa zoezi hilo limekamilika na jumla ya Bandari **437** zisizo rasmi zimetambuliwa ambapo inajumuisha bandari **132** katika mwambao wa Bahari ya Hindi, bandari **204** katika ziwa Victoria, bandari **93** katika ziwa Tanganyika na Bandari **8** katika ziwa Nyasa. Hata hivyo, tayari fedha zinaendelea kukusanywa kutokana na Bandari bubu kwa kutumia vifaa vya POS na mtandao wa POAS ambapo wastani wa **shilingi milioni mia tano (TZS 500,000, 000)** zimekuwa zikipatikana kwa mwezi.

v) Kuhusu Serikali kuhakikisha Viwanja vyote vya Ndege na mali zake zote zinakuwa na Hati Miliki. Kamati imejulishwa kuwa hadi sasa jumla ya Viwanja vya Ndege 12 vimepata Hati Miliki. Hata hivyo, Kamati inaona kasi ya utekelezaji wa ushauri huu si yakuridhisha.

vi) Kuhusu Shirika la Ndege la Tanzania- ATCL kujitangaza kwenye Vyombo rasmi vya Kimataifa ambavyo huonesha safari za ndege dunia nzima. Kamati imejulishwa kuwa, ATCL imeingia kwenye mfumo wa mauzo ya tiketi kimataifa *(Global Distribution System)* ambapo hadi Februari, 2020 imeweza kuuza tiketi katika jumla ya nchi 27 kupitia mfumo huo. Pia imejiunga katika mitandao mikubwa minne (4) ya kuuza tiketi kimataifa ambayo ni *Galileo* uliojikita zaidi katika Bara la Afrika, Amadeus uliojikita zaidi katika Bara la Ulaya na Amerika, Traval Sky uliojikita zaidi katika nchi ya China na Sabre uliojikita zaidi pia katika Bara la Ulaya na Amerika

**b) Sekta ya Ujenzi**

**Mheshimiwa Spika,** katika Sekta ya Ujenzi, ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni;

i) Kuhusu Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) kuharakisha mchakato wa kuchagua karakana za kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri mwendo mrefu kwenda kufanya matengenezo kutokana na Wilaya zingine kuwa umbali mrefu kutoka Makao Makuu ya Mkoa.

Kamati imejulishwa kuwa, Serikali imeelekeza magari yote ya Serikali yatengenezwe katika karakana za Wakala badala ya kupelekwa katika karakana binafsi. Hivyo, Wakala umeanza kutekeleza mpango wa kusogeza huduma zake katika wilaya zilizo umbali mrefu kutoka karakana za mikoa ambapo mwezi Machi, 2020, Wakala ulikuwa umeanzisha karakana mbili (2) katika Wilaya ya Kilombero katika mji wa Ifakara na katika Wilaya ya Kahama. TEMESA inatarajia kuanzisha karakana sita (6) katika Wilaya za Same, Simanjiro, Kyela, Ukerewe, Masasi na Chato.

Aidha, Serikali kupitia TEMESA imeagiza "*Mobile Workshop Truck"* sita na vitendea kazi vyake zitakazotoa huduma katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Tabora, Mtwara, Mbeya na Arusha.

ii) Kuhusu Serikali kuwajengea uwezo wataalam wa ndani katika miradi mikubwa inayotekelezwa, Kamati imejulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya wataalam thelathini na sita (36) kutoka katika Wizara na Taasisi zake wamejumuishwa katika ujenzi wa miradi mikubwa nchini ili kupata mafunzo kwa vitendo kwenye miradi hiyo inayohusu ukarabati wa barabara, madaraja na viwanja vya ndege kupitia *TANROADS Enginering Consulting Unit* (TECU). Aidha, Wahandisi wahitimu 120 wameshikizwa kwenye miradi kwa ajili ya kuwajengea uwezo chini.

Vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na mpango ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikitazamwa kuwa ni kazi za wanaume. Katika mwaka fedha 2020/21 Wizara imepanga kutoa mafunzo kwa makandarasi wanawake ya juu ya kufanya matengenezo na ukarabati wa barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi na

kuwasaidia kusajili kampuni zao za ujenzi pamoja na kufuatilia kwa karibu kazi za barabara zinazofanywa na wanawake wakandarasi.

iii) Kuhusu kununua na kujenga mizani za kisasa ambazo zinapima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo *(Weight in Motion)* na kuzifunga katika maeneo yenye msongamano mkubwa wa kupima magari. Kamati imejulishwa kuwa zimejengwa mizani tano za kisasa zinazopima magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) katika vituo vyenye msongamano mkubwa wa magari vya Njuki (Singida), Nala (Dodoma), Dakawa (Morogoro), Wenda (Iringa) na Mpemba (Songwe).

## c) Sekta ya Mawasiliano

i) Kuhusu ushauri wa kuhakikisha minara yote iliyojengwa kwa ufadhili wa Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) inawekwa mabango yatakayoonesha ushiriki wa Serikali katika uwekezaji huo na kuifanya jamii kutambua mchango wa Serikali katika kusambaza mawasiliano nchini. Kamati imejulishwa kuwa utekelezaji wa ushauri huu umeanza ambapo hadi mwezi Aprili, 2020 minara mia moja na moja (101) iliyopo katika maeneo mbalimbali nchini imewekwa mabango kati ya minara mia saba na nne (704) na zoezi bado linaendelea.

ii) Kuhusu ushauri wa kuongeza rasilimali watu kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF ili Mfuko uweze kusimamia, kukagua na kutembelea ipasavyo maeneo ambayo Serikali imewekeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa Minara na kuhakikisha kazi hiyo imefanyika na mawasiliano yanapatikana kama ilivyokusudiwa. Hatua zimeanza kuchukuliwa ambapo Kamati imejulishwa kuwa kibali cha kuajiri watumishi 21 imetolewa ambapo hadi sasa watumishi 13 wameajiriwa na kuripoti kazini na inatarajiwa ikama iliyoidhinishwa kukamilishwa kwa wafanyakazi wote wapya kujiunga na Mfuko.

iii) Kuhusu kuondolewa kwa Shirika la Posta Tanzania katika orodha ya Mashirika yanayosubiri kurekebishwa ili liweze kutumia rasilimali zilizopo kufanya uwekezaji kwa lengo la kujiendesha kwa tija. Kamati imejulishwa kuwa, Serikali kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imesaini Hati ya kuliondoa Shirika la Posta katika orodha ya Mashirika yanayosubiri kurekebishwa pamoja na kutoa tangazo la Serikali Na. 614 la tarehe 23 Agosti, 2019.

iv) Kuhusu umiliki wa Mikongo binafsi, ambapo baadhi ya Makampuni ya Simu yamekuwa yakimiliki Mikongo yao sambamba na Mkongo wa Taifa, Kamati imejulishwa kuwa Serikali imewasimamisha watoa huduma hao.

v) Kuhusu changamoto ya madeni ambayo TTCL inaidai Serikali na Taasis zake ambapo Kamati imekuwa ikishauri kuweka mikakati ya ukusanyaji wa madeni hayo, Kamati imejulishwa kuwa TTCL imeunda kitengo maalum cha kufuatilia madeni.

## 2.5 Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

### 2.5.1 Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Sekta ya Ujenzi (fungu 98) inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya **shilingi 70,000,000.00** kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Huduma za Ufundi na Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi.

Aidha, kwa upande wa Sekta ya Mawasiliano (fungu 68) inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi 30,000,000,000** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa mawasiliano pamoja na mauzo ya vitabu vya tenda.

### 2.5.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Trilioni 4.9 (4,979,110,240,000.00).**

**Mheshimiwa Spika**, jedwali lifuatalo linaonesha mchanganuo wa fedha zinazoombwa.

**Jedwali Na.2, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida Na Miradi ya Maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

| SEKTA | MATUMIZI YA KAWAIDA | MIRADI YA MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|
| **Ujenzi (Fungu 98)** | 38,774,425,000.00 | 1,766,303,604,000.00 | **1,805,078,029,000.00** |
| **Uchukuzi (Fungu 62)** | 90,710,109,000.00 | 3,067,667,636,000.00 | **3,158,377,745,000.00** |
| **Mawasiliano (Fungu 68)** | 4,654,466,000.00 | 11,000,000,000.00 | **15,654,466,000.00** |
| **JUMLA KUU** | **134,139,000,000** | **4, 844,971,240,000** | **4,979,110,240,000** |

***Chanzo; Taarifa ya Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021***

**Mheshimiwa Spika***,* uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2020/2021 ni yakuridhisha kwani fedha zimeongezeka kwa takribani **Shilingi bilioni 16 (15,813,410,837.00)** ukilinganisha na fedha zilizoidhinishwa mwaka wa fedha **2019/2020** ambazo zilikuwa **Shilingi Trilioni 4.9 (4,963,297,839,163.00)**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuipa kipaumbele sekta ya Miundombinu na kuongeza bajeti ya Sekta hii mwaka hadi mwaka.

## 2.6 Mambo Mengine yaliyojitokeza wakati wa Kupita na Kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2020/2021

### a) Sekta ya Uchukuzi

#### i. Uimarishwaji wa Mtandao wa Reli Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na dhamira ya dhati ya kufufua na kuimarisha miundombinu ya reli nchini ambapo katika kipindi cha miaka mitano yaani 2016 hadi 2020, Serikali imeweka uimarishwaji wa miundombinu ya reli kuwa kipaumbele kikuu kwani imekuwa ikitenga na

kutoa fedha kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa *(standard gauge)*. Ulinganifu wa fedha hizi umekuwa wa kuridhisha ambapo kwa miaka mitano mfululizo zimeidhinishwa na kutolewa takribani jumla ya **Shilingi Trilioni 8** ya fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa. Mchanganuo wa fedha hizi ni kama ifuatavyo; 2016/17 **(Trilioni 1)**, 2017/18 **(Bilioni 900)**, 2018/19 **(Trilioni 1.5)**, 2019/20 **(Trilioni 2.5)** na 2020/21 **(Trilioni 2.1)**.

**Mheshimiwa Spika,** hii ni hatua nzuri na ya kupongezwa kwani, ujenzi wa reli hii yenye kasi ya km 160 kwa saa itasaidia kurahisisha usafiri hasa wa abiria na usafirishaji wa mali ghafi hatimaye kuchochea ukuaji wa viwanda na hata kuongeza Pato la Taifa. *[Utekelezaji wa mradi huu unapatikana katika taarifa ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, kipengele cha 2.3 (ii) na 2.4(i)].*

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa na uwekezaji mkubwa unaofanyika katika reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, ni muhimu pia kuendelea kuboresha na kuimarisha reli ya kati ya zamani *(meter guage).* Katika kufuatilia utekelezaji huu, Kamati imejulishwa kuwa njia ya reli ya kati ya zamani kwa mwaka 2020/2021 ukarabati unaendelea kwa kutandika reli nzito ya ratili 80 kwa yadi katika umbali wa Kilomita 970 kati ya Dar es Salaam na Isaka, ujenzi wa madaraja na makalvati, ujenzi wa sehemu ya kuunganisha treni *(Marshalling yard),* ununuzi wa vifaa ikiwemo ununuzi wa injini 3 na mabehewa 44.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa ukarabati wa njia ya zamani ya kipande cha Tanga-Moshi (350Km) umekamilika na huduma za usafirishaji wa mizigo ulizinduliwa mwezi Julai, 2019. Aidha, Hadi Kamati ilipokutana na Serikali mwezi Machi, 2020 ukarabati wa kipande cha Moshi-Arusha (86Km) umefikia asilimia 95.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu mfuko wa reli ulianzishwa kwa lengo la kuboresha mtandao wa reli ya kati kwa kujenga reli mpya ya standard gauge, kukarabati reli iliyopo na kugharamia tafiti mbalimbali za njia mpya za reli. Katika mwaka 2019/2020 mfuko wa reli ulitengewa jumla ya **Shilingi bilioni**

**255.7** fedha za ndani. Hadi kufikia Februari, 2020, fedha za Mfuko zilizopokelewa ni jumla ya **Shilingi bilioni 159,703.28** sawa na **asilimia 62**.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mfuko wa Reli umetengewa jumla ya **shilingi milioni 289,678.923** fedha za ndani kwa ajili ya kuunda upya vichwa vya treni 9, kurejesha na kuimarisha huduma za usafiri wa treni kwa reli ya Kaskazini (Tanga – Arusha), kugharamia kazi za upembuzi na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli, ukarabati wa karakana, stesheni na majengo ya reli, kuchangia katika kugharamia ujenzi wa reli ya Standard Gauge, na matengenezo ya reli ya kati.

ii. **Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA**

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Mamlaka hii ni kuendeleza, kuendesha shughuli za bandari, kutangaza huduma za bandari, kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa bandari nchini. Kutokana na jiografia ya nchi yetu ambapo imezungukwa na takribani nchi saba ambazo hazina bandari *(land locked countries)* na hivyo kuifanya Mamlaka ya Bandari kutoa huduma kwa mizigo inayoingia na kutoka ndani ya nchi na ya kuelekea nchi za Burundi, Rwanda, DR Congo, Uganda, Zambia, Malawi na Zimbambwe.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo, hatuna budi kuhakikisha kuwa changamoto mbalimbali za miundombinu ya bandari zetu inarekebishwa kwa kufanya ukarabati au kujenga upya. Vilevile kushughulikia changamoto za kiutendaji ambazo zinazorotesha na kusababisha nchi kupoteza wateja waliokuwa wakitumia bandari hususan bandari ya Dar es Salaam na kuhamia katika bandari zingine shindani za Mombasa- nchini Kenya, Beira-nchini Msumbiji, nchini Durban- Afrika Kusini na Walvis Bay-huko Namibia.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ukarabati mkubwa wa miundombinu ya bandari ya Dar es Salaam *[maendeleo ya bandari ya Dar es Salaam yameelezwa katika kipengele cha 2.3 (vi)]* bado upo umuhimu mkubwa wa kuhakikisha bandari zingine kuu na zile za maziwa makuu zinakuwa na mazingira ya miundombinu ya kuridhisha ili kwa pamoja na kwa kushirikiana na bandari ya Dar es Salaam kuweza kusafirisha na kupokea mzigo mkubwa

jambo ambalo litaleta faida kubwa na kuimarisha uchumi wan chi hasa ukizingatia mwelekeo wa Tanzania ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu bandari ya Tanga, kazi ya ukarabati wa gati Namba 2 katika Bandari ya Tanga imefikia asilimia 86. Aidha, kwa upande wa uchimbaji wa kuongeza kina cha kuingilia meli, hadi kufikia Februari, 2020, mradi umefikia asilimia 98 na kutarajiwa kukamilika Machi, 2020. Vilevile, Mamlaka ya Bandari imeendelea na maandalizi ya ujenzi wa gati la kupokelea mafuta kutoka Uganda katika eneo la Chongoleani (Tanga).

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu bandari ya Mtwara, ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 300 linalojengwa kwa ajili ya kuhudumia shehena mchanganyiko limekamilika kwa asilimia 60 na mradi unatarajiwa kukamilika Oktoba,2020. Kukamilika kwa ujenzi wa gati hili kutasaidia sana katika kusafirisha shehena za korosho, makasha, saruji na shehena nyingine zinazotokana na bidhaa zinazotumika katika shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi baharini. Hata hivyo, ni vema mipango ya ujenzi wa magati mengine matatu ikaendelea ili kufungua fursa kubwa zaidi kwa Mtwara kwani itahudumia pia mzigo mkubwa wa wanchi za Malawi na Msumbiji kwani bandari hii ina kina kirefu, eneo kubwa la upanuzi na pia kuwa karibu zaidi na nchi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu bandari za maziwa makuu, miradi ya ujenzi wa magati, majengo ya utawala, majengo ya abiria, kuhifadhia mizigo, uongezaji wa kina, usawazishaji wa eneo, matanki ya maji, vyoo na vyumba vya walinzi zinaendelea kujengwa katika bandari zilizopo katika Maziwa Makuu ambazo ni bandari ya Magarini-Muleba, bandari ya Nyamirembe, bandari ya Lushamba , Bandari ya Karema, Ujenzi wa Gati la Sibwesa/Kalya , Ujenzi wa Gati la Lagosa, Ujenzi wa Gati ya Kabwe – Nkasi , Ujenzi wa Gati za Mbamba Bay, Manda na Matema katika Ziwa Nyasa ambao upo katika hatua ya upembuzi yakinifu. Mingi ya miradi hii inatarajiwa kukamilika mwaka huu 2020.

**Mheshimiwa Spika**, ni muhimu wakati ukarabati na upanuzi wa bandari unaendelea, ni muhimu pia kwa bandari zilizo katika kipaumbele vya Serikali kama vile Bandari ya Mbegani Bagamoyo na Bandari ya Mwambani Tanga

kuanza kutekelezwa. Pia kukamilisha malipo ya fidia kwa wanachi waliopisha upanuzi wa bandari hizi ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima wakati mradi utakapoanza.

iii. **Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwani katika mwaka 2019/2020 imeiwezesha Kampuni ya Huduma za Meli- MSCL kufanya ukarabati mkubwa wa meli mbili za MV Victoria na MV Butiama katika Ziwa Victoria ambazo ukarabati wake unakamilika mwishoni mwa mwezi Machi, 2020. Pia kujenga meli mpya ya kubeba abiria na mizigo inayotarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2021 pamoja na Chelezo katika Ziwa Victoria ikiwa ni nyenzo wezeshi ya kujengea meli na kukarabati meli zilizopo.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020, MSCL ilitengewa **Shilingi Bilioni 70** ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2020 imepokea **Shilingi Bilioni 39** sawa na **asilimia 56** ya fedha zote zilizoidhinishwa. Katika mwaka wa fedha (2020/2021) zimetengwa fedha kiasi cha **Shilingi Bilioni 85** za kufanya ukarabati mkubwa wa meli za MV Umoja, MV Serengeti, MT Nyangumi na MT Ukerewe katika Ziwa Victoria pamoja na Meli za MV Liemba na MT Sangara katika Ziwa Tanganyika na Bahari ya Hindi.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto kwa Kampuni ya Huduma za Meli ni uhaba wa rasilimali watu hususani kada ya watendaji wa melini (mabaharia) ambapo changamoto hii itajitokeza zaidi pindi ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli mbili zitakazokamilika. Uhaba wa vyombo (meli) kwa ajili ya kuhudumia soko kubwa la usafirishaji katika Ziwa Tanganyika na uhaba wa miundombinu kama vile Ofisi kwa ajili ya kuwezesha shughuli za utendaji wa MSCL.

V. **Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kununua ndege kutoka ndege moja iliyokuwepo 2016 hadi kufikia ndege nane. Kuongezeka kwa ndege kumeiwezesha Kampuni ya Ndege ya Tanzania kuongeza mtandao wa safari za ndani ya nchi kutoka vituo tisa (9) hadi vituo kumi na tatu (13) ambapo

kwa sasa inafanya safari katika vituo kumi na moja (11) sababu ya kupisha maboresho ya kiwanja cha ndege cha Mtwara na Songea.

Aidha, ongezeko la ndege limewezesha ATCL kuongeza safari za Kikanda kuelekea Entebe-Uganda, Bujumbura-Burundi, Johannesburg- Afrika Kusini, Harare-Zimbabwe na Zambia-Lusaka. Vilevile, safari za Kimataifa katika vituo vya Bangkok-Thailand, Bombay-India na pia kukamilisha taratibu zote za kuanza safari za kwenda China – Guangzhou ambapo safari zinatarajiwa kuanza kabla ya mwezi Juni, 2020. Changamoto kubwa kwa safari za Kimataifa imekuwa ugonjwa wa Corona unaoenezwa na virusi vya *Covid 19* ambapo imesababisha kusimama kwa safari zote za Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza juhudi hizo mwaka wa fedha 2019/2020 zilitengwa **Shilingi Bilioni 500** ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2020 zimepokelewa **Shilingi Bilioni 310** sawa na **asilimia 62**. Aidha, katika mwaka 2020/21, zimetengwa **Shilingi Milioni 450,000.00** fedha za ndani kwa ajili ya kulipa malipo ya awali ya ununuzi wa Ndege mbili (2) mpya aina ya Boeing 787-8 Dreamliner, kulipa malipo ya awali ya ununuzi wa ndege moja ya mizigo *(freighter)* aina ya Boeing 767-300 na kulipa malipo ya mwisho ya Ndege mbili (2) mpya aina ya Airbus A220-300.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto ya sasa ya ugonjwa wa Corona ambao kwa kiasi kikubwa umeathiri utendaji wa Shirika kwani Shirika limesimamisha safari zake za Kimataifa, Shirika limeendelea kukabiliwa na changamoto ya madeni yaliyolimbikizwa miaka ya nyuma yanayofikia **Shilingi bilioni 180** ambapo katika mwaka wa fedha 2019/20 ATCL ilitengewa **Shilingi bilioni 35.865**. Changamoto nyingine ni ukosefu wa taa za kuongozea ndege katika baadhi ya viwanja vya ndege jambo linalosababisha ndege kutua wakati wa mchana tu.

b) **Sekta ya Ujenzi**

i) **Miradi ya ujenzi wa Barabara**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara ina jukumu la kusimamia ujenzi, ukarabati na matengenezo kwenye mtandao wa barabara kuu na za Mikoa zenye urefu wa jumla ya kilomita 35,000 ambapo kati ya hizo kilomita 12,786 ni barabara kuu na kilometa 22,214 ni barabara za mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara ziweze kupitika kwa urahisi na hatimaye kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi kama ilivyofafanuliwa katika Mipango Mikakati ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

**Mheshimiwa Spika**, Sekta hii kwa sasa inakabiliwa na changamoto ya mvua kubwa zinazoendelea kunyesha nchini mfululizo ambazo kwa kaisi kikubwa zimesababisha mafuriko ambao yameharibu sana barabara na madaraja. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 fedha za dharura zilikuwa zimekadiriwa jumla ya **Shilingi bilioni 15.** Katika mwaka wa fedha 2020/2021 zimetengwa jumla ya **Shilingi Bilioni 28.2** kwa ajili ya matengenezo ya dharura ya barabara. Kamati ianipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake na kuongeza fedha za dharura.

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa barabara nchini (TANROADS) umeendelea kukabiliwa na changamoto ya fedha za miradi ya maendeleo kutolewa kwa kiasi kidogo au kutokutolewa kwa wakati na hivyo kusababisha baadhi ya Makandarasi kusimama kufanya kazi na wengine kutekeleza kazi kwa kasi ndogo jambo ambalo linasababisha baadhi ya miradi kutokamilika katika muda uliokusudiwa. Hadi kufika mwezi Machi, 2020 baadhi ya miradi ya barabara ilikuwa haijapata fedha ni Dar es Salaam-Chalinze-Morogoro Express Way, barabara ya Korogwe-Handeni, Mwanza -Shinyanga Boarder, Arusha - Namanga, Singida –Babat i-Minjingu, Same-Mkumbara-Korogwe.
Aidha, baadhi ya barabara fedha zilitolewa ni kidogo ukilinganisha na kiasi kilichoidhinishwa na muda uliobaki kabla ya kumaliza mwaka wa fedha 2019/2020. Barabara hizo ni Dodoma -Iringa, Handeni –Kibereshi -Kibaya-

Singida, Kitumbi- Segera- Tanga, Msimba- Ruaha Mbuyuni-Mafinga, Kisarawe - Mlandizi, Ipole -Rungwa na Magole-Mziha-Handeni.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, lengo mojawapo la Sekta ya Ujenzi ni kuhakikisha Miji yote Mikuu na Mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami. Hata hivyo, bado kuna Mikoa mingine ambayo haijaunganishwa kwa barabara za lami hususan Mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Rukwa, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera, Mbeya –Makete- Njombe, Lindi- Morogoro, Lindi-Ruvuma, Arusha-Mara, Singida-Mbeya, n.k. Aidha, baadhi ya barabara za Mikoa ziko katika hali isiyoridhisha na nyingine hazipitiki wakati wa mvua hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii.

ii) **Malipo ya Makandarasi na Wahandisi Washauri**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na makandarasi na Wahandisi Washauri katika ujenzi hususan kwenye miradi ya barabara. Kamati imejulishwa kuwa hadi kufikia Februari, 2020 Serikali imetoa kiasi cha **Shilingi bilioni 615,449,139,848.53**. Aidha, deni la Makandarasi na Wahandisi Washauri wa miradi ya barabara ni **Shilingi bilioni 950**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwashirikisha makandarasi wa ndani katika ujenzi wa miradi ya barabara ambapo kiasi cha **Shilingi milioni 403,164.774** za Mfuko wa barabara zimetumika kuwalipa makandarasi wa ndani. Aidha, kuhusu changamoto ya makandarasi wa ndani kuwa na uwezo mdogo wa mtaji hivyo kushindwa kushiriki kikamilifu katika fursa za kazi kutokana na masharti ya upatikanaji wa dhamana za zabuni, dhamana za ushiriki wa kazi na mitaji ya kuwezesha kufanya kazi kutoka mabenki. Kamati imejulishwa kuwa Bodi imeendelea kuendesha Mfuko wa kusaidia Makandarasi –*Contractors Assistance Fund*-CAF ambao unatoa dhamana za zabuni na malipo ya awali kwa makandarasi wa ndani walio katika daraja la chini na la kati. Mfuko umeendelea kuwa na mtaji wa **Shilingi bilioni 3.75** kwa mwaka 2019/2020. Aidha, idadi ya wanachama imepungua kutoka 1,186 mwaka 2018/2019 hadi kufikia 1,126 mwaka 2019/2020. Idadi ya wanachama imepungua kutokana na zoezi la kufuta makandarasi waliokosa sifa kwa mujibu wa sharia.

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Februari, 2020 Bodi ya Usajili wa makandarsi imesajili makandarasi wapya 508 na hivyo kufanya jumla ya makandarasi waliosajiliwa kufikia 10,822. Aidha, jumla ya miradi 2,065 ilikaguliwa ambapo miradi 548 sawa na asilimia 27 ilipatikana na mapungufu mbalimbali ambapo makandarasi waliokutwa na mapungufu walichukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutozwa faini, kupewa onyo, kusimamishwa kufanya biashara ya ukandarasi na kufutiwa usajili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuwapa kipaumbele makampuni na wahandisi wazawa kwani Kamati imejulishwa kuwa hadi mwezi Februari 2020, jumla ya wahandisi waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali ni 27,739 na makampuni ya kihandisi kuwa 359 ambapo wahandisi 25,401 ni Wahandisi wa ndani na 2,338 ni wahandisi wa kigeni. Aidha, makampuni ya ushauri wa kihandisi ya kizalendo ni 246 na ya kigeni ni 113.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Serikali inawapa kipaumbele makandarasi na wahandisi pamoja na Makampuni yao ya ndani katika utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini. Hili ni jambo jema kwani fedha na malipo mbalimbali yanayofanyika hubaki katika mzunguko wa fedha nchini na kusaidia kuinua pato la mtu mmoja mmoja na hata Taifa,

iii) **Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)**

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya Wakala wa Nyumba Tanzania ni pamoja na usimamizi na uendeshaji wa Miliki yote ya Serikali (Viwanja/maeneo ya Ardhi yaliyotengwa kwa matumizi ya Serikali, Majengo ya Ofisi za Taasisi mbalimbali za Serikali, Nyumba za Viongozi wa ngazi za juu Serikalini, Nyumba za kuwauzia Watumishi wa Umma, Nyumba za kupangisha, pamoja na uwekaji wa samani bora kwenye nyumba za Viongozi) na utoaji wa huduma za ushauri na ujenzi wa majengo ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwani kwa kupitia Wakala wa Majengo Tanzania-TBA imeweza kufanikisha miradi mbalimbali mikubwa kama vile ujenzi wa Ofisi za Serikali Mtumba-Dodoma, Ujenzi wa Nyumba za

Magomeni Kota na ujenzi na ukarabati wa nyumba za viongozi pamoja na watumishi wa umma nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wakala huu, Wakala umekuwa unakabiliwa na changamoto kubwa ya malimbikizo ya madeni ya ujenzi, ushauri, pango la nyumba pamoja na mauzo ya nyumba. Kwa kiasi kikubwa Wakala unazidai Wizara, Idara pamoja na Taasisi za Serikali ambapo hadi mwezi Machi, 2020 madeni yaliyohakikiwa na kuwasilishwa Hazina ili yalipwe ni jumla ya **shilingi bilioni 17**.

Changamoto zingine ni pamoja na mahitaji makubwa ya nyumba za watumishi wa umma ukilinganisha na kasi ndogo ya ujenzi, riba kubwa kwenye taasis za fedha, kasi ya mabadiliko ya teknolojia katika vifaa, mbinu na ubunifu kwenye sekta ya ujenzi inaugharimu Wakala fedha nyingi za kuwapatia mafunzo wataalam wake ili waendane na mabadiliko hayo na vifaa vya ujenzi vyenye gharama kubwa katika soko kusababisha kuongeza gharama za ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imebaini changamoto vongozi wengi wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kukaimu nafasi zao za uongozi. Hali hii hairidhishi na inasababisha viongozi hao wasijiamini katika kufanya maamuzi muhimu ya taasisi.

iv) **Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (*The Tanzania Electrical Machanical and Electronics Services Agency-TEMESA*) ni Wakala muhimu sana kwani unatoa huduma ya matengenezo ya magari, mitambo, pikipiki, mifumo ya umeme, majokofu na viyoyozi. Vilevile Wakala huu unasimamia ukodishaji wa magari na mitambo ya kusaga kokoto pamoja na kutoa ushauri katika nyanja mbalimbali za kihandisi Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwani imeelekeza magari yote ya Serikali kutengenezwa katika karakana za TEMESA badala kupelekwa katika karakana binafsi ambazo zilikuwa ni za gharama kubwa. Hata hivyo, ili utekelezaji huu ufanyike ni muhimu

sana kwa Wakala kukamilisha kusogeza karibu karakana zake ikiwa ni pamoja na mobile workshop truck, kuajiri wataalam waliobobea katika ufundi wa magari, vifaa na mitambo ya kisasa pamoja na kuboresha mazingira ya karakana.

v) **Miradi ya Ujenzi wa Viwanja vya Ndege**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha sekta ya usafiri wa anga, pamoja na ununuzi wa ndege, miradi mbalimbali ya ujenzi wa viwanja vya ndege inaendelea katika Mikoa mbalimbali kama vile Kigoma, Mpanda, Mtwara, Mwanza, Bukoba, Kilimanjaro, Arusha, Sumbawanga, Shinyanga, Kilimanjaro, Msalato, Tabora na Songwe na viwanja vya ndege vya Mikoa.

**Mheshimiwa Spika**, miradi hii inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti na kutokutolewa fedha kwa wakati. Katika mwaka wa fedha 2019 /2020, jumla ya **Shilingi 102,192,375,000.00** zilitengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa **Shilingi 40,000,000,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 62,192,375,000.00.** Hadi kufika mwezi Februari, 2020 jumla ya **Shilingi 61,205,521,015.40** ndizo zilizokuwa zimetolewa sawa na **asilimia 61** ya fedha zote za miradi ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege. Kati ya fedha hizo zilizotolewa fedha za ndani ni **Shilingi 8,413,556,960.18** sawa na **asilimia 21**. Kwa upande wa fedha za nje zilizotolewa ni **Shilingi 52,791,964,055.22** sawa na **asilimia 85**.

**Mheshimiwa Spika,** fedha zilizotolewa hadi Febrari, 2020 ni kidogo ukilinganisha na miradi iliyokuwa imepangwa kutekelezwa ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kati ya miradi kumi na tatu (13) ya viwanja vya ndege iliyokuwa imeidhinishiwa fedha 2019/2020, ni miradi minne tu (4) tu ndio iliyopata fedha ambayo ni Kiwanja cha Ndege cha Mtwara, Msalato, Mwanza na Jengo la tatu la abiria-kiwanja cha Julius Nyerere Dar es Salaam. Miradi ambayo haikuwa imepata fedha ni Kiwanja cha ndege cha Kigoma, Mpanda, Shinyanga, Tabora, Sumbawanga, Songwe, Arusha, Kilimanjaro na Bukoba.

c) **Sekta ya Mawasiliano**

i) **Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imejulishwa kuwa TCRA imeendelea na ujenzi wa mifumo na uratibu wa huduma za Mawasiliano kwa kutumia mtambo wa Mfumo wa kusimamia mawasiliano ya simu *(Tele-Traffic Management System-TTMS)*, ambao umechangia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni zilizopo katika udhibiti wa mawasiliano na kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki kutokana na huduma za mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai,2019 hadi Januari, 2020 Mfumo wa TTMS pamoja na mambo mengine umewezesha kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha mtandao kwa mashirika yote ya simu ambapo jumla ya miamala 2,004,196,139 imepita katika mitandao ya simu na wastani wa fedha zilizopita ni **Shilingi 12,202,700,000,000**.

Aidha, katika mwaka huu wa fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2020, mapato kutokana na Mtambo wa *TTMS* ambayo yamelipwa katika mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi 7,275,340,578.44**. Kwa ujumla Mfumo huu umeongeza ufanisi katika usimamizi wa Sheria ikiwa ni pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya kasi yanayotokea katika Sekta ya Mawasilinao duniani.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu usajili wa laini simu, Mamlaka ya Mawasiliano kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano imeendelea na zoezi la usajili wa laini za simu kwa njia ya biometria ambapo hadi Machi, 2020 zimesajiliwa laini 35,813,455 sawa na asilimia 83.1 ya laini zote 43,072,868 zilizounganishwa mtandaoni. Aidha, kwa upande wa laini zilizozimwa hadi kufikia tarehe 10 Machi, 2020 ni laini 5,886.286. Laini ambazo bado hazijasajiliwa kwa alama za vidole lakini zilisajiwa kwa kitambulisho cha mpiga kura na kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi ni 7,259,413.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa zoezi la usajili wa namba za simu ni endelevu kwani mahitaji ya kuwa na laini ya simu kwa ajili ya mawasiliano yataendelea kuwepo siku hadi siku, na kutokana na changamoto iliyojitokeza ya wananchi wengi kutokufikiwa ama kutokufanikisha usajili kutokana na kukosa vitambulisho

vya Taifa toka NIDA na hivyo kusababisha wananchi wengi kusajili laini kwa kuazima vitambulisho ni jambo ambalo si sahihi. Ni vema sasa Mamlaka ya Mawasiliano kwa kushirikiana na NIDA pamoja na watoa Huduma kuendelea kuhamasisha na kutoa elimu ili wananchi wasajili laini za simu kwa kutumia vitambulisho vyao.

iii) **Mradi wa Postikodi na Misimbo za Posta**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni muhimu sana kwani ni mradi ambao utarahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa kuweza kufanyika kwa urahisi na kuokoa muda. Miongoni mwa huduma zitakazorahisishwa na kuwapo kwa mfumo huu ni pamoja na; huduma za umeme, gesi, maji, mabenki, ulinzi, usafiri na usalama, huduma za dharura kama zima moto, magari ya wagonjwa, pamoja na wasambazaji wa vifurushi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na umuhimu wa mradi huu, bado kumeendelea kuwapo changamoto ya kutokutolewa fedha za mradi kwa wakatai au fedha za mradi kutokutolewa kabisa. Kwa miaka minne mfululizo mwenendo wa utoaji fedha katika mradi huu sio wa kuridhisha. Katika mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi huu uliidhinishiwa **shilingi bilioni 3** ambapo kiasi kilichotolewa kilikuwa **milioni 95** tu; katika mwaka wa fedha wa 2017/18 iliidhinishiwa **shilingi billion 3** ambapo hadi kufikia Machi 2018, hakuna kiasi chochote kilichotolewa. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 iliidhinishiwa **shilingi bilioni 4** lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2019 kiasi kilichopokelewa ni **shilingi milioni 796** na mwaka wa fedha 2019/2020 mradi huu haukutengewa fedha, hata hivyo Kamati ilijulishwa kuwa fedha za maendeleo ya mradi huu zingetolewa katika fedha za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano jambo ambalo halikufanyika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati haioni dhamira ya dhati ya Serikali katika kutekeleza mradi huu ukilinganisha na umuhimu wake kwa Taifa.

iv) **Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (USCAF)**

**Mheshimiwa Spika,** lengo la kuanzishwa kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(Universal Communication Service Access Fund- UCSA*F ni kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara ambapo usambazaji wa

Mawasiliano unafanywa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa kushirikiana na sekta binafsi hususan Makampuni ya simu kama vile TIGO, VODACOM, HALOTEL.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mawasiliano kwa wote toka kuanzishwa kwake umefanikiwa kupeleka huduma za mawasiliano katika kata 704 zenye Vijiji 2,501 na wakazi zaidi ya milioni tano. Serikali kupitia UCSAF mnamo mwezi Januari, 2020 imesaini mkataba na makampuni ya simu ili kupeleka huduma za mawasiliano katika kata 252 zenye vijiji 555 na wakazi zaidi ya milioni tatu ifikapo ifikapo mwezi Oktoba, 2020.
Hata hivyo, pamoja na mafaniko hayo ya usambazaji wa mawasiliano nchini, Kamati imebaini changamoto kubwa ni upungufu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kusambaza mawasiliano katika maeneo yenye uhitaji wa huduma hizo kwa wakati.

v) **Shirika la Mawasiliano Tanzania – TTCL**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha miaka minne, kumekuwepo na juhudi mbalimbali za kuhakikisha TTCL inamudu ushindani wa kibiashara na kuzidi kuimarika. Jitihada hizo ni pamoja na Serikali kununua hisa asilimia 35 zilizokuwa zinamilikiwa na Kampuni ya *Bhart Airtel;* Serikali kuridhia kubadilisha deni ililokuwa inaidai TTCL kiasi cha **Shilingi bilioni 76.6** kuwa mtaji wa Shirika; Serikali kuchukuwa deni la ada ya udhibiti ambalo TTCL ilikuwa ikidaiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzani Tanzania- TCRA kiasi cha cha **shilingi bilioni 25**; TTCL kuruhusiwa kutumia rasilimali zake kama dhamana ya mkopo ambapo Shirika limechukuwa dhamana ya mkopo benki ya **Shilingi bilioni 66** kati ya **Bilioni 96** na kuwekeza katika teknolojia ya 4G LTE ya simu za mkononi; TTCL kupewa kipaumbele wakati wa kugawa masafa; na TTCL kupewa majukumu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya sekta ya mawasiliano kama vile Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kupeleka mawasiliano vijijini kutoka Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote(UCSAF).

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 20019/2020, Shirika lililkuwa limekadiria kuzalisha na kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi Bilioni 196.8 (196,832,435,039)** kutokana na huduma za Shirika kama vile simu, data na kupangisha maeneo kwa ajili ya vyombo vya mawasiliano. Hata hivyo, uchambuzi

wa Kamati umebaini kuwa makadiria hayo hayakufikiwa kwani Shirika hadi mwezi Februari, 2020 limekusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 60.1 (60,137,125,692.84)** sawa na **asilimia 30.5.** Kamati imefahamishwa kuwa sababu za TTCL kutokufikia lengo la makusanyo ni kutokana na kukosa fedha kwa ajili ya uwekezaji kutoka kwenye vyanzo vyake ikiwemo mkopo kutoka benki. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2020/2021, TTCL inatarajia kukopa kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 15** kwa ajili ya uwekezaji ambao utaliwezesha Shirika kuongeza Mapato.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hali ya utendaji wa Shirika la Mawasiliano Tanzania-TTCL bado si yakuridhisha kwani bado Shirika linakabiliwa na changamoto ya mtaji mdogo wa uwekezaji usiyoendana na mabadiliko ya teknolojia na kushindwa kukabiliana na ushindani wa soko la Mawasiliano. Changamoto zingine zinazolikabili Shirika la Mawasiliano Tanzania ni pamoja na: -

a) Madeni ya zamani ambayo yanatokana na kutumia huduma mbalimbali ambayo mengi yao Shirika linaidai Serikali na Taasis zake ambapo hadi mwezi Machi, 2020 kiasi cha **Shilingi bilioni 30** zinadaiwa;

b) Kutokukamilika kwa Kanuni ambazo zitatoa maelekezo ya namna ya Shirika kuendesha na kusimamia miundombinu ya kimkakati ya mawasiliano;

c) Shirika kuwa na mtaji mdogo kwa ajili ya uwekezaji na kushindwa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia yanayokwenda sanjari na kasi ya uwekezaji;

d) Sheria ya manunuzi kwa mashirika ya umma ambayo inaleta urasimu unaokinzana na ushindani wa kibiashara; na

e) Uharibifu na ukataji wa miundombinu ya Mkongo unaotokana na shughuli za binadamu, hujuma, na shughuli za maendeleo kama ujenzi na upanuzi wa barabara.

vi) **Shirika la Posta Tanzania –TPC**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka utaratibu wa kupeleka fedha kwa Shirika la Posta kwa kila kipindi cha miezi mitatu kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika

Mashariki ambapo deni hilo hadi kufikia mwezi Januari 2020 limebaki **Shilingi bilioni 6,521,748,190**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Serikali kupitia Sheria ya Msamaha *(Amnesty)* kufuta deni la Shirika la **Shilingi Bilioni 12** lililokuwa limetokana na tozo, riba, na adhabu. Kamati bado inaona umuhimu wa Serikali kufuta deni lililosalia la takribani **Shilingi bilioni 15** ili kupunguza mzigo wa madeni kwa Shirika na kwa kuzingatia kuwa Shirika hili bado linakabiliwa na changamoto ya kuwa na mtaji hasi na hivyo kushindwa kumudu ushindani uliopo kayika huduma ya kusafirisha barua, vipeto na rejesta ndani na nje ya nchi.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Bajeti ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha mwaka hadi mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kwa miaka minne mfululizo Sekta hii imekuwa ikitengewa fedha kiasi cha kuridhisha ambapo mwaka 2017/2018 **Shilingi trillioni 4.5**, 2018/2019 **Shilingi trilioni 4.2,** mwaka 2019/2020 **Shilingi trilioni 4.9** na kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 **Shilingi trilioni 4.9**. Kwa kuangalia fedha hizo zilizoidhinishwa ndani ya miaka mine mfululizo, ni dhahiri kuwa, Serikali imeipa kipaumbele cha kutosha sekta ya miundombinu nchini ili kuharakisha maendeleo ya nchi. Hivyo, Kamati inazidi kusisitiza ushauri wake kuwa fedha zinazoidhinishwa zitolewe kwa wakati ili kuhakikisha miradi inatekelezwa katika muda uliopangwa na hatimae wananchi wananufaika.

### 3.2 Sekta ya Uchukuzi

1. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa reli nchini Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa;
    a) Ujenzi wa reli ya kati uende sambamba na ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni, ili mradi utakapokamilika mnamo mwezi June, 2020 kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro huduma za usafirishaji zianze kufanyika;

    b) Serikali kuzingatia kuwaajiri wahandisi wakutosha wa ndani wenye fani mbalimbali muhimu na zinazohitajika kwa uendeshaji wa reli pamoja na kutoa mafunzo mbalimbali ya uendeshaji wa treni na uratibu wa matumizi ya reli mpya ili mradi utakapokamilika pawepo na wataalam wa ndani ambao watakuwa tayari kuupokea na kuusimamia vizuri;

    c) Ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya reli na kuondoa usumbufu kwa wananchi, Shirika la Reli Tanzania-TRC liweke alama zinazoonesha mwisho wa eneo la reli ili kuondoa usumbufu kwa wananchi;

d) Shirika la reli lianze kujiendesha kisasa kwa kufunga vyombo vya kielektroniki ili kuweza kutunza kumbukumbu zote za kiutendaji, ufatiliaji wa mizigo kwa wateja, uthibiti wa mafuta, udhibiti wa mwendo na usalama. Hii italifanya Shirika hili kuweza kujiendesha kisasa na kupunguza gharama za uendeshaji;

e) Juhudi ziendelezwe kuhakikisha ujenzi wa reli nchini unafanywa kwa ushirikiano na sekta binafsi au mikopo yenye gharama nafuu kwani itasaidia kuharakisha zoezi zima la ujenzi wa reli nchini na Serikali itaweza kuweka fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo.

2. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Bandari Kamati inashauri yafuatayo;

a) Serikali kwa kupitia Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Viwanda na Biashara waitishe kikao cha pamoja na wadau mbalimbali wa bandari nchini ili kubadilishana mawazo na kuona namna nzuri ya uendeshaji wa bandari nchini na kuifanya bandari iweze kujiendesha kibiashara na kuvutia wafanyabiashara wengi kuitumia jambo ambalo litaongeza mapato ya Serikali;

b) Serikali iharakishe kukamilisha bandari za nchi kavu katika maeneo ya Kwala -Pwani, Ihumwa -Dodoma, Fela-Mwanza, Katosho-Kigoma, King'ori-Arusha, Isaka-Kahama, na Inyala- Mbeya ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar es salaam kwa ajili ya kutoa mizigo;

c) Sulala la wadau wote wa bandari kuhamia kwenye jengo moja liwe jambo la lazima ili kurahisisha na kuongeza ufanisi wa bandari;

d) Serikali iharakishe kutafuta mwekezaji ili ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo uweze kuanza. Vile vile, Serikali ilipe fidia kwa wananchi

waliobakia ndani ya eneo linalotarajiwa kujengwa bandari hii ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima wakati mradi huu utakapoanza;

e) Ni muhimu sana Serikali kuhakikisha mwezi Juni, 2020 kama ilivyoeleza katika taarifa za utekelezaji wake kuwa inakamilisha mchakato wa kupata *flow meter* na kuifunga katika bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia Bandari ya Dar es Salaam. Na kwakuwa imeelezwa kuwa zimeagizwa *flow meter* zingine mbili za bandari ya Tanga na Mtwara, ni muhimu nazo zikamilishwe na kufungwa kwa muda ili kuweza kujua kwa uhakika kiwango cha mafuta kinachoingia bandarini;

f) Kuhusu Bandari ya Mtwara, kasi ya uanzishwaji wa bandari ya hii iende sambamba na ujenzi wa njia ya treni; na

g) Kwakuwa Serikali sasa imerasimisha bandari bubu na kuanza kukusanya mapato, ni vema na muhimu kuboresha mazingira ya miundombinu ya bandari hizo ili umuhimu wa urasimishaji na mapato yanayopatikana yaweze kuonekana kwa uhalisi wake kwa wamiliki na watumiaji wa bandari hizi.

3. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Kampuni ya Huduma za Meli-MSCL; Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali ijipange kutengeneza meli zote kumi na nne (14) zilizopo katika Maziwa Makuu ili kuiwezesha Kampuni ya Meli Tanzania kumudu kujiendesha kibiashara;

b) Kutokana uwekezaji unaofanyika sasa wa kukarabati na ujenzi wa meli mpya katika Maziwa Makuu, ni vema Serikali iendelee kulipa mishahara ya kwa wafanyakazi wa Kampuni ya Meli Tanzania hasa kwa kipindi hiki cha mpito mpaka Kampuni hii itakapoweza kujiendesha; na

c) Serikali iharakishe ujenzi wa meli katika ziwa Tanganyika na kukarabati meli iliyopo ya MV Liemba kwani kijiografia bandari hii inapakana na nchi

ya Kongo (Rubumbashi) ambako kuna mizigo mkubwa wa biashara ambao utaiwezesha Serikali kupata mapato.

4. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu TAZARA, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali iharakishe mazungumzo baina ya nchi wabia wa reli ya TAZARA kuhusu kuimarisha reli hii kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi. Serikali kwa kushirikiana na nchi wabia wa TAZARA ikamilishe itifaki ya 16 kuhusu mkopo kutoka china kwa ajili ya kusaidia kuiboresha TAZARA;

b) Serikali ikamilishe manunuzi ya injini na vipuri pamoja na mitambo ya kusaidia kuzalisha kokoto na mataluma ya zege kwenye mgodi wa kokoto uliopo Kongolo- Mbeya na kusaidia viweze kuingia nchini kwa haraka ili vianze kutumika kwa ajili ya kuongeza pato la TAZARA;

c) Serikali iharakishe mchakato wa ajira za watumishi wa TAZARA ili kupata wafanyakazi wenye ujuzi na weledi wa kutosha kuliongezea Shirika uwezo kwani wafanyakazi wengi wamemaliza muda wao na kustaafu;

d) Serikali ihakikishe inatoa kwa wakati fedha za ujenzi wa kipande cha reli chenye urefu wa kilometa 18 kutoka Chikola kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kuipatia TAZARA mapato ya kutosha; na

e) Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kulipa madeni yote ya wafanyakazi wastaafu wa TAZARA.

5. **Mheshimiwa Spika,** kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA: -

a) Kamati inaendelea kushauri Serikali kuipatia Mamlaka hii angalau **asilimia 50** ya maduhuli yatokanayo na viwanja vya ndege ili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege- (TAA) iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuongeza kasi ya ujenzi na ukarabati; pamoja na,

uendeshaji wa viwanja vya ndege nchini. Aidha, Mamlaka izitumie vizuri fedha za mapato ya ndani zinazotokana na utuaji wa ndege, uegeshaji wa ndege na magari katika maegesho ya viwanja ili ziweze kutumika katika shughuli za uendeshaji wa viwanja vya ndege;

b) Serikali ihakikishe Viwanja vyote vya Ndege na mali zake zote zinakuwa na Hati Miliki; Aidha, kuhakikisha Viwanja vya Ndege vyote vinawekewa uzio kwa ajili ya kuepusha hatari zinazotokana na wanyama au binadamu wanaokatiza katika maeneo ya viwanja vya ndege pamoja na; kuepuka migogoro ya ardhi na wananchi wanaoishi pembezoni mwa viwanja hivyo; na

c) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) na wadau wengine wa viwanja vya ndege kama Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), wafanye vikao vya pamoja na kuangalia namna ya kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili katika sekta ya usafirishaji wa anga.

6. **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania-ATCL

a) Japokuwa Kamati imefahamishwa kuwa kwa sasa ATCL imekuwa na marubani wa kutosha ambapo marubani 78 wamehitimu mafunzo na kupata sifa stahiki za kuendesha ndege. Ni muhimu sana kwa Serikali kuweka mikakati ya kuhakikisha inalinda marubani wake wasichukuliwe na mashirika mengine;

b) Wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL kupewa mafunzo ya huduma kwa wateja, mara kwa mara, ili kuweza kutoa huduma nzuri wakati wote. Hii itasaidia Kampuni kushindana na makampuni mengine yanayofanya biashara ya usafiri wa anga; na

c) Shirika liendelee kufanya utaratibu wa kuongeza safari za ndani na za kikanda ili kuimarisha mtandao wa safari zake.

### 3.3 Sekta ya Ujenzi

1) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Wakala wa Barabara- TANROADS, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri ufuafuatao: -

   a) Serikali itekeleze Sera yake ya kuunganisha Mikoa yote kwa barabara za lami. Baadhi ya Mikoa hiyo ni Lindi –Morogoro, Morogoro -Mlimba -Madeke Njombe, Lindi –Songea, Kigoma –Katavi-Tabora-Kagera, Mbeya –Makete -Njombe, Arusha–Mara. Aidha, miradi ya barabara inayoendelea ipewe kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembuzi yakinifu;

   b) Serikali ijenge kwa kiwango cha lami barabara muhimu zifuatazo: -

      i. Barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi nyigine hususani Mikoa ya Kagera, Kigoma, Katavi, Ruvuma na Mtwara;
      ii. Barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa kama vile Kigoma-Kasulu-Kagera, Katavi – Kigoma – Tabora;
      iii. Barabara za Kiuchumi, kama vile, Mtwara – Newala – Masasi, ambayo ni barabara inayopita katika maeneo ambayo yanazalisha korosho kwa wingi ukizingatia kwamba zao la korosho linachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa mikoa ya kusini na nchi kwa ujumla; barabara ya Handeni – Kibereshi -Kibaya– Singida ambayo ni barabara yenye tija kiuchumi kutokana na kuwapo kwa bomba la mafuta linalounganishwa na nchi ya Uganda. Aidha, umuhimu wa makubaliano ya nchi ya Rwanda kutaka kutumia bandari ya Tanga;
      iv. Barabara zinazounganisha Wilaya na Makao Makuu ya Mikoa, hizi pia zipewe kipaumbele ili kuwezesha wakulima kuweza kuyafikia masoko ya mazao; na
      v. Barabara zilizohaidiwa za Marais waliostaafu na Rais aliye madarakani.

   c) Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kuendelea kutoa mafunzo kwa wahandisi washauri na Makandarasi wa ndani ili waweze kusimamia na kutekeleza ujenzi wa barabara kikamilifu. Aidha, kuhamasisha wakandarasi wazalendo kujiunga na kuomba zabuni kwa utaratibu wa ubia na kupata dhamana kupitia

mfuko Maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia makandarasi wadogo na wa kati. Vilevile, kuhamasisha zaidi kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa Wahandisi na Makandarasi wanawake.

d) Sekta ya Ujenzi isimamie ipasavyo Sheria ya barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari, kama runinga, magazeti, redio na simu za mkononi. Aidha, vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na kubomolewa mapema. Aidha, Wakala wa Barabara iendelee na zoezi la kuweka alama za mipaka katika maeneo ya barabara ili kuepusha usumbufu wakati maeneo hayo yanapohitajika;

e) Serikali iendelee na juhudi kufunga mizani ya kisasa zinazopima magari huku yakiwa kwenye mwendo katika vituo ambavyo vinamsongamano mkubwa wa magari kwenye mizani ili kuokoa muda, fedha na usumbufu kwa wasafiri na wasafirishaji;

f) Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi ambavyo vinajengwa katika Ukanda wa Kati na Ukanda wa Dar es Salaam ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa pamoja na kuokoa muda wa mizigo kukaa barabarani;

g) Wakati wa ujenzi wa barabara ni vema wakala wa barabara wahakikishe wanaweka sehemu maalum kwa ajili ya kuvukia mifugo, kwani, maeneo mengi ambayo mifugo inatumia kuvuka kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa barabara;

h) Wakati wa ujenzi wa barabara zipo taasisi nyingi za Serikali zinapeleka madai kwa wakandarasi wa barabara kwa ajili ya ulipiaji malighafi zinazotumika kwenye ujenzi, kama vile Wizara ya Madini (kokoto, mawe, kifusi), Wizara ya Maji na umwagiliaji (vima vya maji), Wizara ya Viwanda na Mazingira (uharibifu wa mazingira); pamoja na, ushuru unaotozwa na Halmashauri za miji; gharama hizi zinaongeza gharama za ujenzi wa

barabara, hivyo, Kamati inaishauri Serikali isamehe kodi hizo kwani zinalipwa na Serikali na si wakandarasi; na

i) Serikali ihakikishe inaweka mikakati ya kupunguza msongamano ya magari kwenye miji inayokua kwa kasi, kama vile, Mbeya, Mwanza, Arusha na hivi sasa Dodoma. Miji hii imekuwa ikikabiliwa na msongamano mkubwa wa magari na kusababisha kutumia muda mwingi kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine

2) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa viwanja vya ndege, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali ikamilishe kwa haraka ujenzi unaoendelea wa kiwanja cha ndege cha Mwanza hasa ujenzi wa jengo la abiria, mizigo; pamoja na jengo la kuongozea ndege;

b) Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa ajili ya ujenzi wa Viwanja vya Ndege ili miradi hii iweze kukamilika kwa wakati na kuepuka riba ambazo hutokana na miradi kutokamilika kwa wakati;

c) Ni muhimu Serikali iharakishe kujenga na kuimarisha Viwanja vya Ndege vitakavyozalisha mapato na kujiendesha; kama vile, Kiwanja cha Ndege cha Moshi (kwa ajili ya utalii), Kiwanja cha Ndege cha Iringa (kwa ajili ya Utalii) na Kiwanja cha Ndege cha Mtwara (kwa ajili ya uwekezaji);

d) Serikali ilipe fidia mapema na kwa wakati kwa wananchi wanaopisha ujenzi mathalani kiwanja cha Ndege cha Msalato, Songea, Lake Manyara, Simiyu na Msalato; na

e) Serikali iweke taa za kuongozea ndege hususan katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma na Songwe-Mbeya ili ndege ziweze kutua na kuruka wakati wote.

3) **Mheshimiwa Spika,** kuhusu Wakala wa Ufundi na Umeme- TEMESA, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Wakala uendelee kukamilisha mchakato wa kuchagua karakana za kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri umbali mrefu kwenda kufanya matengenezo;

b) Wakala uchukue hatua za makusudi na kuweka mkakati wa kudumu ili kukusanya madeni yake ambayo, kwa kiasi kikubwa, inazidai taasisi za Serikali ili Wakala huu uweze kijiendesha kibiashara badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini; na

c) Serikali iajiri wataalam waliobobea kwenye fani ya ufundi wa magari na kuhakikisha kunakuwa na mitambo ya kisasa ili kuendana na kukua kwa teknolojia kwani mara nyingi magari ya Serikali yamekuwa yakitengenezwa kwenye karakana binafsi za mitaani jambo ambalo si sahihi;

## 3.4 Sekta ya Mawasiliano

1) **Mheshimiwa Spika,** kuhusu mradi wa Anuani Makazi na Misimbo ya Posta, Kamati inasisitiza ushauri ufuatao; -

a) Serikali itoe kipaumbele kwa mradi wa anwani za makazi na misimbo ya posta kwani mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, Kamati inashauri Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa;

b) Ili mradi huu uwe wa kisasa na kuendana na wakati, ni vema wataalam wakajifunze nchi zingine na kuona namna nchi nyingine zilivyofanya na kuweka mfumo huu; na

c) Wakati zoezi la kuweka majina ya mitaa linaendelea, ni muhimu Serikali za Mitaa kuhakikisha zinaweka ulinzi wa nguzo dhidi ya wahalifu wanaochukua vyuma chavu.

2) **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA, Kamati inashauri; -

a) Kamati inaendelea kusisitiza kuongezwa kasi ya zoezi la usajili wa namba za simu ili kuwa na taarifa za kila mmiliki au mtumiaji wa simu kwa ajili ya usalama na kutekeleza Sheria ya Mawasiliano na Posta. Vilevile, Serikali iongeze kasi ya kutoa vitambulishao vya Taifa ili kila Mtanzania aweze kutambuliwa na kuepuka udanganyifu unaofanywa kwenye mitandao;

b) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA, ikabiliane na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, ambapo kumekuwa na ongezeko la uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi zikae pamoja na kuona namna ya kushughulikia changamoto ya uhalifu wa kimtandao na kuwasaidia wananchi kuwabana wahalifu bila ya kuwa na urasimu;

c) Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania isimamie Makampuni ya Simu nchini na kudhibiti gharama za mitandao, kwani gharama za baadhi ya mitandao zipo juu ukilinganisha na mitandao mingine; na

d) Kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao na kuimarisha usalama wa watu na mali zao.

3) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa: -

a) Serikali ipitie na kuangalia upya taratibu za umilikishwaji ardhi hasa maeneo ya ardhi yanayojengwa minara ili kuweka utaratibu wa maeneo yaliyokodiwa ama kununuliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara kumilikiwa na Serikali za vijiji husika. Hii itasaidia kwani fedha zitakazopatikana kutokana na malipo ya kukodi ama kununua eneo la mnara zitatumika kwa maendeleo ya wananchi walio wengi tofauti na ilivyo sasa ambapo maeneo mengi yaliyojengwa minara yananufaisha watu wachache na baadhi ya Serikali za vijiji kutokuambulia chochote;

b) Serikali iweke mpango wa uwiano wa mawasiliano nchi nzima hasa maeneo ya mipakani ambapo mara nyingi watu katika maeneo hayo hupata mawasiliano ya nchi jirani jambo ambalo linawakosesha haki ya kukosa taarifa za nchi yao;

c) Serikali izipe kipaumbele na kuhakikisha kunawekwa minara ya mawasiliano Wilaya na Halmashauri mpya zote;

d) Serikali ihakikishe inasimamia kuwepo kwa ushirikiano katika mifumo ya miundombinu (*Infrastructure Sharing)* na kuyaelekeza makampuni ya simu kushirikiana katika ujenzi wa minara na kufunga antenna zao katika mnara mmoja ili kuepuka matumizi ya eneo kubwa la ardhi kwa kuwa mlundikano wa minara katika eneo moja;

e) Halmashauri na Serikali za vijiji zitoe ushirikiano wa kutosha na wa haraka pale ambapo maeneo yanahitajika kwa ajili ya ujenzi wa minara ili kuweza kurahisisha kupata mawasiliano kwa haraka;

f) Mfuko wa Mawasiliano kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa fedha na kuhakikisha miradi mingi inatekelezwa na kufikia maeneo mengi yenye uhitaji wa mawasiliano kama ilivyopangwa;

a) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote utoe elimu kwa wananchi ili wajue umuhimu na uwekezaji unaofanywa na Serikali katika kuleta maendeleo hususan katika ujenzi wa minara ya mawasiliano ili wananchi watoe ushirikiano wa ulinzi ili vifaa vya minara view salama;

b) Kuongeza rasilimali watu kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili Mfuko uweze kusimamia ipasavyo kwa kukagua na kutembelea maeneo ambayo Serikali imewekeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa minara na kuhakikisha kazi hiyo imefanyika na mawasiliano yanapatikana kama ilivyokusudiwa; na

c) Kwa kuwa teknolojia imeendelea na wananchi wengi wamekuwa na mwamko katika huduma za TEHAMA; na hivyo, kuhitaji huduma ya *data (mtandao)*. Ni muhimu sana, minara yote iliyojengwa na inayoendelea kujengwa iwe na

uwezo wa 3G na 4G tofauti na ilivyo sasa katika viwango vya 2G ambayo inanyima wananchi wengi fursa ya huduma ya data ambayo ingeweza kurahisisha huduma za afya (afya mtandao), elimu mtandao n.k

d) Serikali ifanye jitihada za kuweka na kusambaza mawasiliano nchini katika maeneo mengi zaidi hasa mipakani kwani mawasiliano ni maendeleo na hasa sasa ambako nchi yetu inawekeza katika viwanda. Kuwepo kwa mawasiliano kutarahisisha usafiri na uuzwaji wa malighafi na mazao hata kuinua kipato cha Mwananchi mmoja mmoja na hata Taifa kwa ujumla;

4) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Shirika la Posta Tanzania, Kamati inashauri Serikali iendelee kulipa madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuliondolea Shirika mzigo wa kulipa deni hilo kila mwezi, fedha ambazo zingeelekezwa kwenye uendeshaji wa shirika.

5) **Shirika la Simu Tanzania- (TTCL Corporation)**

a) Pamoja na TTCL kuunda kikosi cha kufuatilia madeni ambayo yameripotiwa hadi tarehe 30 Machi, 2020 kufika Jumla ya **Shilingi Bilioni 30** ambayo kwa kiasi kikubwa zinadaiwa Wizara/Taasisi na Mashirika ya Serikali, Kamati inaona mkakati huu bado hautakuwa na nguvu ikiwa Serikali yenyewe haijweka mkazo kwa vyombo vyake kulipa madeni hayo. Hivyo, ni muhimu sana kwa Serikali kuchukuwa hatua na kusisitiza vyombo vyake kulipa madeni ya mawasiliano yanayodaiwa na TTCL.

b) Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhakikisha kunakuwa na mpango endelevu wa kuulinda na kuuendeleza Mkongo wa Taifa;na

c) Kwa kuwa TTCL ni Shirika la Umma, lipewe Mamlaka ya kumiliki na kuendesha Mkongo wa Taifa badala ya ilivyo sasa ambapo Mkongo unasimamiwa na kuendeshwa na TTCL lakini mapato yake yanaelekezwa Wizarani.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, sekta ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ni muhimu sana katika kuharakisha na kuchochea maendeleo ya nchi. Miradi iliyo ndani ya Sekta hii ni mikubwa na inahitaji fedha nyingi ili yote iweze kukamilika kwa wakati uliopangwa. Hivyo, Kamati inaona ni muhimu Serikali kushirikisha Sekta binafsi katika kutekeleza miradi hii mikubwa.

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti pamoja na kuandaa taarifa hii. Naomba kuwatambua wajumbe wa Kamati hii kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb- M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Eng. Ramo Matala Makani, Mb
4. Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwako, Mb
5. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb
6. Mhe. Joyce John Mukya, Mb
7. Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb
8. Mhe. Susan Chogisasi Mgonukulima, Mb
9. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb
10. Mhe. Nuru Awadhi Bafadhili, Mb
11. Mhe. James Francis Mbatia, Mb
12. Mhe. Saul Henry Amon, Mb
13. Mhe. Ahmed Makbhuty Shabiby, Mb
14. Mhe. Dkt. Chuachua Mohamed Rashid, Mb
15. Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mb
16. Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb
17. Mhe. Dua William Nkurua, Mb

18. Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb
19. Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga, Mb
20. Mhe. Rukia Kassim Ahmed, Mb
21. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb
22. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb
23. Mhe. Munde Abdalah Tambwe, Mb
24. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb
25. Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb

**Mheshimiwa spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na Ushauri kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kwa namna ya pekee naomba niwashukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Eng. Isack Alloyce Kamwelwe, (Mb) akisaidiana na Manaibu Mawaziri Mhe. Justus Atashasta Nditiye, (Mb) na Mhe. Elias John Kwandikwa, (Mb).

Aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii Arch. Elius A. Mwakalinga (Sekta ya Ujenzi), Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Katibu Mkuu Mtsaafu Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano) pamoja na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Jim Yonaz. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Vilevile, shukrani ziende kwa watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu. Michael Lucas Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu. Gerald Singano Magili pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John Mvunta na Ndugu Janeth Julian Malangu, Msaidizi wa Kamati Ndugu. Modesta Michael Kipiko pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Seleman Kakoso, Mb

**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA MIUNDOMBINU**

4 Mei, 2020

***KIAMBATISHO NA.1,* Gharama zilizolipwa na zinazodaiwa na Wakala wa Majengo za Ada ya Ushauri kwa Wizara na Taasisi zilizojenga Ofisi Mtumba, Dodoma**

| NA | WIZARA | MKANDARASI | GHARAMA (TSHS) | ADA YA USHAURI | Kiasi kilicholipwa | Kiasi kinachodaiwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MAMBO/ NJE | CSWS-Arusha | 973,032,900.00 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 2 | MALI ASILI | SUMA-North | 999,242,000.00 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 3 | ARDHI | NHC | 998,800,850.00 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 4 | VPO | CSWS-Dodoma | 883,913,500.00 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 5 | FEDHA | NHC | 999,891,770.27 | 54,832,452.71 | 54,832,452.71 | - |
| 6 | KILIMO | SUMA-Lake | 998,428,150.00 | 54,832,453.71 | - | 54,832,453.71 |
| 7 | TAMISEMI | MUST | 2,600,000,000.00 | 86,024,566.52 | - | 86,024,566.52 |
| 8 | PMO-SERA | MZINGA | 978,277,356.20 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 9 | MAJI | SUMA-South | 998,000,000.00 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 10 | UJENZI | CSWS-DSM | 983,437,600.00 | 82,231,968.00 | 82,231,968.00 | - |
| 11 | UTUMISHI | TBA | 996,953,685.60 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 12 | AG CHAMBERS | CSWS-Mwanza | 970,000,000.00 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 13 | MADINI | MZINGA | 975,360,028.10 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 14 | HABARI | MZINGA | 978,277,356.20 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 15 | NISHATI | NHC | 997,955,322.00 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 16 | VIWANDA | NHC | 998,800,850.00 | 54,832,452.71 | 52,090,830.07 | 2,741,622.64 |
| 17 | SHERIA | SUMA-Eastern | 999,909,000.00 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 18 | ULINZI | SUMA-Eastern | 997,751,000.00 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 19 | MIFUGO | SUMA-Central | 996,000,000.00 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 20 | MAMBO/ NDANI | PRISONS | 992,131,895.00 | 54,832,452.71 | - | 54,832,452.71 |
| 21 | ELIMU | PRISONS | 988,136,895.00 | 78,342,956.65 | 57,164,156.32 | 21,178,800.33 |
| 22 | AFYA | MZINGA | 975,360,028.10 | 54,832,452.71 | 52,090,830.00 | 2,741,622.71 |
| 23 | PMO-KAZI | PRISONS | 994,815,000.00 | 69,637,050.00 | 69,637,050.00 | - |
| 24 | TARURA | MUST | 2,600,000,000.00 | 189,472,500.00 | 39,856,893.75 | 149,615,606.25 |
| 25 | EGA | WATUMISHI | 960,642,650.00 | 160,815,719.63 | 40,000,000.00 | 120,815,719.63 |
| **JUMLA TSHS** | | | **27,835,117,836.00** | **1,708,341,363.29** | **447,904,180.85** | **1,260,437,182.44** |

***Chanzo***; *Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Majengo Tanzania, Machi 2020*